



وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنْكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لِيَسْتَخْلِفُنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا أَسْتَخْلَفْتُ  
الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ وَلَمْ يُكَفِّرُنَّهُمْ لَهُمْ أَنْقَعُنِي لَهُمْ وَلَمْ يُكَفِّرُنَّهُمْ مِنْ بَعْدِ خَرْقِهِمْ أَنَّا  
يَعْبُدُونِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمِنْ كُفَّارَ بَعْدِ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّاغِنُونَ

Ijumaa, 1 Rabi' II 1446 H

04/10/2024 M

Na: HTS 1446 / 12

### Tanzia ya Mbebaji Ulinganizi

(Imetafsiriwa)

Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema:

[وَلَنَبْلُونَكُمْ بِشَيْءٍ مِنَ الْخَوْفِ وَالْجُوعِ وَنَقْصٍ مِنَ الْأَمْوَالِ وَالْأَنْفُسِ وَالثُّمَرَاتِ وَبَشَرَ الصَّابِرِينَ \* الَّذِينَ إِذَا أَصَابَتْهُمْ مُّصِيبَةٌ قَالُوا إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعُونَ \* أَوْلَئِكَ عَلَيْهِمْ صَلَوَاتٌ مِنْ رَبِّهِمْ وَرَحْمَةٌ وَأَوْلَئِكَ هُمُ الْمُهَنَّدُونَ]

"Hapana shaka tutakujaribuni kwa chembe ya khofu, na njaa, na upungufu wa mali na watu na matunda. Na wabashirie wanao subiri, Wale ambaao ukiwasibu msiba husema: Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu, na kwake Yeye hakika tutarejea. Hao juu yao zitakuwa baraka zitokazo kwa Mola wao Mlezi na rehema. Nao ndio wenye kuongoka." [Al-Baqrah:155 - 1].

Baada ya kukubali Qada'a ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir katika Wilayah Sudan yamuomboleza:

**Sheikh Alim Ahmad Al-Hussein Muhammad Ahmad Mudawi**

Mmoja wa Mashababu wake aliyebeba Dawah ya kurudisha maisha kamili ya Kiislamu kuitia kusimamisha Khilafah Rashida ya pili kwa njia ya Utume, akistahamili madhara ya madhalimu jeuri mpaka yakini ilipomjia jana, Alhamisi, tarehe 30 Rabi ' al-Awwal 1446 H, sawia na 3/10/2024, kwenye Kisiwa cha Tuti jijini Khartoum.

Mwenyezi Mungu amrehemu Sheikh Alim Abu Abdul Mun'im, amsamehe, na amjaalie Firdaws ya juu katika Jannah.

Ajaaliye kaburi lake liwe bustani mionganoni mabustani ya Jannah. Alijulikana kwa kufunga na kusimama katika swala, kipenzi mionganoni mwa watu wake, kiasi ambacho walikuwa wakisema kuwa yeye ni Swahaba. Alikuwa mkarimu na mtukufu.

Macho yanabubujika machozi, moyo unahuzunika, na tumehuzunishwa sana na kuondoka kwako, ewe Abu Abdul Mun'im, lakini hatusemi ila tu yale yanayomridhisha Mola wetu:

[إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعُونَ] "Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu, na kwake Yeye hakika tutarejea." [Al-Baqra:156].

Rambirambi zetu ziende kwa familia yake, jamaa na ndugu zake katika Dawah.

**Ibrahim Othman (Abu Khalil)  
Msemaji Rasmi wa Hizb ut Tahrir  
katika Wilayah Sudan**